MWONGOZO WA KUONGOZA

Jinsi ya kutumia 'Somo Hili La Biblia'

Somo hili La Biblia humpatia Kiongozi jinsi rahisi ya kuongoza kikundi chake kusoma Bibilia kupitia majadiliano. Urahisi na kina cha somo hizi huwapa watu wa umri tofauti na viwango tofauti vya Imani motisha wa kuchambua Biblia kibinafsi na kwa vikundi vidogo vodogo.

Somo hili La Biblia ni mwongozo wa kila siku wa wahusika kukamilisha kwa ubinasfi kupitia kufungu kimoja cha Bibilia ili kujitayarisha kwa mkutano na majadiliano ya kikundi katika wiki inayofuatia.
Wahusika husoma kifungu walichopewa kila siku, kisha kuomba wapate ufunuo na kukamilisha maswali ya kila siku.
Kila siku, Roho Mtakatifu hutoa ufunuo wa kina na kuvumbua maana zaidi ya kifungu hicho.
Wahusika hupata mazoea ya kusoma neno la Mungu, kuvumbua ukweli wa Mungu walioupokea, na kutumia ukweli huo kupitia njia rahisi ifuatayo ya kusoma Bibilia:

- **Maono**:
  Somo linasema mambo gani?
  Lengo lake ni lipi?
- **Utabiri**:
  Somo lina maana gani?
  Ni maneno gani, vipengele vipi na ukweli upi muhimu?
- **Matumizi:**
  Ni kwa jinsi gani Roho Mtakatifu ananiongoza kutumia somo hili maishani?

Jinsi Ya Kuanzisha Kikundi Cha Kusoma Bibilia

Tuna amini kwamba Mwenyezi Mungu angependa kukutumia wewe jinsi ulivyo na mahali unapo ishi, unapofanya kazi na unako jumuika na watu, ili kutimiza mambo makuu ya milele.
Ili kuanza, tizama orodha hii ya mambo matatu rahisi:

1. OMBA

... huanza kwa maombi na uhusiano

MAOMBI

- Muombee mwenzako atakaye kusaidia kuanzisha kikundi cha Somo hili La Bibilia.
- Ombeni pamoja mara kwa mara. Muulize Mungu awape mpango wake na mwelekeo.
- Waombeeni watu kwa kutaja majina yao. Ombeni Mumgu awape fursa za kupatana nao, kuwajali na kuwatumikia
- Waombeeni wapate hamu ya kusoma Bibilia.

UHUSIANO

- Kutana na majirani wako wanao ishi, wanao fanya kazi na wanao jumuika karibu na wewe. Kuwa rafiki mwema kwao na uwape motisha.
- Anzisha mazungumzo – waulize maswali na uwape sikio lako (skiza kwa umakini).
- Jumuikeni pamoja kwa kikombe cha chai, kahawa au chakula.
- Tafuta fursa ya kuonyesha upendo na kuwatumikia.

2. UNGANA

... watafute walio na hamu ya kujiunga

PANGA MKUTANO

- Panga siku, saa na kikao cha mkutano.
- Tengeza orodha ya wale wangependa kuhudhuria mkutano.
- Omba, kisha uwaalike.
- Fanya mpango wa kuandaa kiburudisho kama ingewezekana.
- Tengeza orodha ya mpangilio wa mkutano (mambo ya kufanya kwenye mkutano).

MUONGOZO WA MKUTANO

- Kama inahitajika, andaa kiburudisho kama chai, kahawa au matunda.
- Wakaribishe walio hudhuria na ujitambulishe ili muweze kujuana. Jumuika pamoja kwa kuulizana maswali, kuimba nyimbo, au michezo ya ucheshi ili kujuana zaidi.
- Mnapo malizia mkutano, wapongeze wageni kwa kuhudhuria. Unaweza ukatumia maneno yafuatayo kwa hotuba yako: *"Umekua wakati mzuri sana kwetu sisi kujumuika pamoja. Ni matumaini yangu na lengo langu kuona sisi kama jamii tuki ishi kwa umoja na upendo, na kusoma Bibilia pamoja ili kuelewa jinsi inavyosema, na kupata ufunuo wa kuelewavile la Mungu linatushusu sisi binafsi. Je, wewe ungependa kushuhudia mambo haya?"*

ONGOZA

… sasa anza.

- Pakua na uchapishe Mwongozo wa Kusoma na umpe kila mtu nakala yake.
- Chagua somo moja la Bibilia kati ya sehemu nne za **Maandiko Yaliyopendekezwa** katika Mwongozo huo wa Kusoma.
- Wahusika watahitaji kijitabu kidogo cha kunakili kurasa walilosoma kibinafsi kila wiki.
- Mkutano wa kwanza wa somo la Bibilia:

- Someni kwa pamoja somo la wiki ya kwanza kisha mjadiliane maswali ya siku tano za wiki kama kikundi. Hii itaonyesha jinsi ilivyo rahisikutumia somo la kibinafsi na itawezesha kiongozi kuongoza mjadala wa Bibilia kulingana na majibu ya washirika.
- Wapatie washirika somo la wiki ya pili na uwahimize kukamilisha maswali ya siku tano za wiki, kabla ya wiki ifuatayo.

Jinsi ya kuongoza kikundi cha somo la Bibilia

Anza kwa maombi

- Uliza mmoja wa washirika ajitolee kusoma kifungu cha somo.
- Ongoza majadiliano kutoka kwenye maswali ya kila siku yaliyo kwenye Mwongozo wa Kusoma.

Usitie shaka kama watu watakimya unapo subiri majibu. Lengo ni kuwa na majadiliano, wala sio kiongozi kuyajibu yale maswali.

Wakumbushe washirika baadhi ya mipangilio muhimu ili kuwa na majadiliano yenye mwafaka:

- Zungumza kwa sauti ya juu ili kusikika vizuri na watu wote.
- Jibu kwa ufupi tu, bila kutumia maneno mengi.
- Hakikisha majadiliano yana angazia Yesu Kristo na mambo ya Bibilia.
- Toa mwelekeo mkamilifu na uhakikishe kakuna majadiliano ya kisiasa.

Waeleze wahusika ya kwamba Roho Mtakatifu atatumia neno lake, mambo ambayo kila mhusika anayoyapitia maishani, kiwango chao cha Ukristo na kuwafunza kwa ubinafsi yale mambo angependa wajue na kuyatenda maishani.

- Katika mwisho wa somo, wape somo la wiki inayofuatia.
- Wahimize kuwakaribisha washurika wengine kujiunga na somo hili la Bibilia. Hii huwafanya watu kuhisi jamii inayowajali na iko na ukarimu.
- Hitimisha mkutano kwa maombi.

Maswali zaidi ambayo yangeweza naweza fanya somo liwe la kufana.

- Ni mambo gani mengine Mwenyezi Mungu alikufunza?
- Unaweza ukafanua jibu lako zaidi?
- Waulize washirika, ni mambo gani wangependa kuongeza kwenye jibu hilo.
- Ni jambo gani lililokupendeza sana kuhusu kurasa ou somo hilo?

Utangulizi:

Aina wengi wa kasa wa bahirini wako katika hali ya hatari. Hii si kwa sababu ya wnayama wanowala, binadamu, ama kuzorota kwa mazingira; ila ni kwa sababu ya mwangaza usio wa kiasili unaopatikana kwenye ukingo wa bahari.

Mungu aliwaumba kasa wa baharini ili wawe wanazaliwa wakati wa mwezi mpevu. Kasa wanapoangua, mwangaza wa mwezi huwaongoza katika makaazi yao ya kiasili – baharini. Maisha ya kasa wa bahirini yamo majini.

Watafiti walishangaa kupata kasa wachanga wakiwa wamekufa kwenye mwisho wa vinjia vya zigizagi vilivyokuwa katikati ya njia iliyo angaziwa na mwezi na zile za mwangaza wa bandia zilizotoka kwa nyumba za pwani, taa, na trafiki. Usumbufu kutokana na ile miangaza bandia

ndio ulielekeza hao kasa kwenye vifo vyao.

Mwanagaza Masomo ya Biblia ya Siku Tano yatakuvutia kwenye mnato wa mwangaza wa Yesu. “Mimi ndio mwangaza wa dunia…mwangaza inaoelekeza kwenye uhai” (Yohana 8:12). Pia yatakuvutia kwa Neno Lake – “Neno Langu ni mwangaza miguuini pako na mwangaza kwa njia yako” (Zaburi 119:105) na pia kukuwezesha kuwa mwangaza wa Kristo kwa ulimwengu wa giza “Nyinyi ni nuru ya dunia … ng’aeni kwa wote waone” (Mathayo 5:14).

Kila siku unaposoma, angazia, na utekeleze Neno la Mungu kwa maisha yako, utakuwa na uwezo zaidi wa kutambua miangaza bandia ya adui, bakia kwa njia iliyo angaziwa na Mungu, na ung’ae kwa mwanagaza mkali kwa ajili ya Kristo, jamaa yako na jamii. Chambua masomo manne ya Mwangaza unaozingatia uhai, mahusiano, miujiza, na jumbe za Yesu.

MWANGA © 2017 NBS2GO. Haki zote zimehifadhiwa. Imechapishwa kwa Kiingereza kwa LIGHT © 2016 NBS2GO.
Ilitafsiriwa na kiutamaduni ilichukuliwa na NBS2GO. http://www.nbs2go.com